



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BENKI KUU YA TANZANIA



3 Julai 2025

TAARIFA YA KAMATI YA SERA YA FEDHA

Katika kikao chake kilichofanyika jana, tarehe 2 Julai 2025, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) iliamua kupunguza Riba ya Benki Kuu kutoka asilimia 6.00 hadi asilimia 5.75. Hivyo, Benki Kuu itatekeleza sera ya fedha ili kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki (7-day interbank rate) inabaki ndani ya wigo wa asilimia 3.75 hadi 7.75.

Uamuzi huu unaakisi imani ya Kamati katika mwenendo wa mfumuko wa bei ambao umeendelea kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3–5, na matarajio yanayoonesha kuendelea kuwa tulivu ndani ya wigo huo. Hali hii inatokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kuanza kwa msimu wa mavuno, pamoja na utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania. Ingawa migogoro ya kisiasa duniani na ongezeko la ushuru wa bidhaa za forodha umeongeza sintofahamu kwenye mwenendo wa uchumi wa dunia, mazungumzo na makubaliano ya hivi karibuni yanaashiria hatari hizi zinaweza kupungua.

Kamati ya Sera ya Fedha pia ilipitia mwenendo wa uchumi wa ndani na kubaini kuwa umeendelea kuimarika kwa kasi ya kuridhisha, ukichochewa na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika miundombinu na kuongezeka kwa shughuli za sekta binafsi, kutokana na kuimarika kwa mazingira ya ufanyaji biashara. Hatari za misukosuko ya nje kwenye matarajio ya mwenendo uchumi ni ndogo, kutokana na muundo wa uchumi wetu wenye kutegemea sekta mbalimbali za uzalishaji, pamoja na utekelezaji thabiti wa sera na programu zinazochochea ukuaji wa uchumi, ambazo zinatarajiwa kusaidia kuhimili misukosuko hiyo. Tathmini ya Kamati kuhusu mwenendo wa uchumi wa dunia na wa ndani pamoja na matarajio ya baadaye imebainishwa kama ifuatavyo:

1. Tathmini ya Kamati ya mwenendo wa uchumi wa dunia na matarajio ya baadaye, inabaini kuongezeka kwa hali ya sintofahamu kwenye mwenendo wa uchumi na biashara duniani, kutokana na kuongezeka kwa migogoro ya kisiasa duniani na ushuru wa forodha. Hali hii imechangia kudhoofisha matarajio ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2025. Hivyo basi, ukuaji wa uchumi kwa robo ya pili ya mwaka 2025 ulikuwa na mwenendo tofauti baina ya nchi, huku nchi chache tu duniani zikiimarika kiuchumi.

2. Mfumuko wa bei umepungua katika nchi nyingi, kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha inayopunguza ukwasi katika kipindi cha nyuma na kushuka kwa bei za chakula na nishati. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kushuka, ingawa kwa kasi ndogo kuliko ilivyotarajiwa awali, kutokana na kutotabirika kwa sera za uchumi na biashara duniani. Bei za bidhaa katika soko la dunia zilikuwa na mwenendo tofauti. Bei ya dhahabu iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani 3,282.40 kwa wakia mwishoni mwa Juni 2025 kutoka dola za marekani 2,855.73 mwishoni mwa Machi 2025, kutokana na kuongezeka kwa migogoro ya kisiasa na mivutano ya kibiashara duniani, ambayo imepelekea ongezeko la mahitaji ya dhahabu kama rasilimali salama ya uwekezaji na kuweka akiba. Kwa upande mwingine, bei ya mafuta ghafi ilipungua hadi dola za marekani 65.92 kwa pipa kutoka dola za marekani 74.35, kutokana na kupungua kwa mahitaji duniani na kuongezeka kwa usambazaji kutoka nchi wanachama wa OPEC+. Hivyo basi, benki kuu nyingi duniani zinatarajiwa kutekeleza kwa umakini sera za fedha, huku zikijaribu kudhibiti hatari zinazoweza kuongeza mfumuko wa bei, sambamba na kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi.

3. Uchumi wa ndani uliendelea kuwa stahimilivu na unatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukuaji wa uchumi kwa Tanzania Bara unakadiriwa kufikia asilimia 5.8 katika robo ya kwanza na asilimia 5.5 katika robo ya pili ya mwaka 2025. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na sekta za kilimo, ujenzi na huduma za fedha na bima. Uchumi wa ndani unatarajiwa kuendelea kuimarika, ambapo ukuaji wake unatarajiwa kufikia asilimia 6.0 na 6.9 katika robo ya tatu na ya nne, mtawalia. Uchumi wa Zanzibar pia unatarajiwa kufuata mwelekeo huu. Kasi hii ya ukuaji inachochewa na uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya reli, barabara, viwanja vya ndege, na viwanja vya michezo kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya CHAN na AFCON, pamoja na uwekezaji unaoendelea katika sekta za kilimo na madini. Matarajio haya chanya yanathibitishwa pia na matokeo ya tafiti za Mtazamo wa Masoko na Maoni ya Watendaji Wakuu wa Kampuni (*Market Perception Survey and CEOs Economic Perception Survey*) zilizofanyika mwezi Mei 2025. Imani ya wawekezaji pia imeendelea kuimarika, kama inavyoonekana kwenye matokeo ya tathmini iliyofanywa na Kampuni ya Fitch mwezi Juni 2025, iliyothibitisha daraja la B+ kwa Tanzania, ikiwa na mwelekeo thabiti.

4. Mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara ulikuwa wastani wa asilimia 3.2 katika robo ya pili ya mwaka 2025, ukiakisi utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na utulivu wa bei za bidhaa zisizo za chakula na zile za nishati. Hata hivyo, mfumuko wa bei za chakula uliongezeka kidogo, kutokana na changamoto za usafirishaji zilizosababishwa na mvua kubwa katika baadhi ya maeneo. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei ulipungua hadi asilimia 4.2 mwezi Mei 2025, kutoka asilimia 5.3 mwaka mmoja uliopita, hali iliyochangiwa zaidi na kushuka kwa bei za chakula.

5. Ujazi wa fedha uliendelea kuongezeka kwa kasi ya kuridhisha, ukiakisi ongezeko la mahitaji ya shughuli za kiuchumi. Ujazi wa fedha (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 19.1 kwa mwaka

katika robo ya pili ya mwaka 2025, ikilinganishwa na asilimia 15.4 katika robo ya kwanza. Ukuaji huu ulitokana kwa kiasi kikubwa na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, iliyokua kwa asilimia 16.7, ikiashiria kuimarika kwa upatikanaji wa mitaji na mazingira ya biashara. Sekta ya fedha iliendelea kuwa imara na thabiti. Sekta ya benki imeendelea kuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha, na yenye kutengeneza faida. Ukuaji wa amana na utoaji mikopo ulichangiwa na kuongezeka kwa mtandao wa huduma za mawakala wa benki na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma. Uwiano wa mikopo chechefu (NPLs) ulipungua hadi asilimia 3.4 mwezi Mei 2025, ukiwa chini ya kiwango cha juu kinachovumilika cha asilimia 5. Mwenendo huu unaashiria kuongezeka kwa ubora wa mikopo na kuimarika kwa usimamizi madhubuti wa vihatarishi katika sekta ya benki.

6. Utekelezaji wa sera ya bajeti kwa Tanzania Bara na Zanzibar ulichangia kufikia malengo ya utekelezaji wa sera ya fedha. Makusanyo ya mapato yalifikia malengo yaliyowekwa, yakichangiwa na uboreshaji wa usimamizi wa kodi na kuongezeka kwa ulipaji kodi kwa hiari. Matumizi yaliendana na rasilimali zilizopo, jambo linalioashiria umakini wa Serikali katika utekelezaji wa bajeti. Kamati ya Sera ya Fedha ilibaini kuwa utekelezaji madhubuti wa sera ya bajeti sambamba na maboresho yanayofanyika, yatachangia ukuaji endelevu wa uchumi na kusaidia sera ya fedha katika kuhakikisha mfumuko wa bei unakuwa mdogo na tulivu. Deni la Serikali liliendelea kuwa himilivu, ndani ya viwango vinavyokubalika kimataifa.

7. Sekta ya nje iliendelea kuimarika katika robo ya pili ya mwaka 2025, ambapo nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilikadiriwa kupungua hadi kufikia dola za Marekani milioni 797.1 katika robo ya pili ya mwaka 2025, kutoka dola za Marekani milioni 872.1 katika robo ya pili ya mwaka uliopita. Katika mwaka 2024/25, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida unakadiriwa kuwa asilimia 2.6 ya Pato la Taifa (GDP), ikipungua kutoka asilimia 3.7 mwaka uliotangulia, ikichangiwa na ongezeko la mauzo ya bidhaa nje ya nchi ikiwemo, dhahabu, utalii, mauzo ya bidhaa za viwandani na mazao ya biashara. Kwa upande wa Zanzibar, urari wa malipo ya kawaida unakadiriwa kufikia ziada ya dola milioni 611.1 kwa mwaka 2024/25, ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 428.5 mwaka uliopita, ukichangiwa na ongezeko la mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha, ikikadiriwa kufikia takribani dola za Marekani bilioni 6, ikiwa ni kiwango cha juu kufikiwa kwa hivi karibuni. Akiba hii inatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kwa takribani miezi 4.8. Sekta ya nje inatarajiwa kuendelea kuimarika tunapoelekea kwenye msimu wa mauzo ya bidhaa na huduma, hususan utalii, mazao ya biashara na dhahabu.

8. Shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa tulivu dhidi ya sarafu nyingi za kigeni. Thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilishuka kwa kasi ndogo ya asilimia 0.2 kwa mwaka ulioishia Juni

2025, ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 12.5 katika kipindi kama hicho mwaka jana. Utulivu huu umechangiwa hasa na kuongezeka kwa ukwasi wa fedha za kigeni kutokana na mapato ya utalii, na mauzo ya bidhaa nje ya nchi, hususan dhahabu na tumbaku. Aidha, utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na usimamizi wa Kanuni zinazotaka miamala ya fedha ya ndani ya nchi kufanyika kwa shilingi vimechangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha utulivu wa shilingi. Vilevile, ongezeko la ununuzi wa dhahabu kutoka ndani ya nchi kwa ajili ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni lilichangia kuongeza imani kwa sarafu ya Tanzania.

9. Maelezo ya kina ya tathmini ya mwenendo wa uchumi na mwelekeo wake yatapatikana katika Ripoti ya Kamati ya Sera ya Fedha (MPC Report) inayopatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu <https://www.bot.go.tz/Publications/Filter/49>. Kamati ya Sera ya Fedha inatarajia kukutana tena tarehe 1 Oktoba 2025, na tangazo la CBR litafanyika tarehe 2 Oktoba 2025.

Kamati ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania hukutana kila robo mwaka, kutathmini mwenendo na mwelekeo wa uchumi na kuamua Riba ya Benki Kuu. Riba hii hutoa mwelekeo wa Sera ya fedha, wenye lengo la kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la muda wa kati, la asilimia 3 hadi 5 na kuchangia ukuaji endelevu wa uchumi.

**EMMANUEL M. TUTUBA
GAVANA**